

KUTOA PRESHA



... kuhesabiwa miongoni mwa kundi kama hili, kuwa hapa asubuhi ya leo tena. Na Ndugu Shakarian. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Bwana aliyaokoa maisha yake. Hakika nilishangaa kusikia habari zake. Lakini nina furaha sana kwamba jambo tunalohubiri, pia linafanya kazi miongoni mwetu, ku—kuona ya kwamba Mungu huwaponya wagonjwa na wanaoteseka.

Nasi tuna dakika chache tu, na yapata dakika mbili za kuzungumza, halafu ningetaka kuwaombea wale walio kwenye nchi ya redio, na walio wahitaji.

² Ndio kwanza tuondoke Pines ya Kusini, Carolina ya Kaskazini ambako Bwana alifanya mwujiza mkuu. Usiku mmoja tulipokuwa tukiingia, muda ulikuwa umeenda sana kwa maskini huyo mama aliyekuwa amewasili na mtoto mchanga mwenye kichwa kilichojawa maji kupata kadi ya maombi na kuingia mstarini, lakini alikuwa amesimama nyuma ya mapazia pamoja na mtoto huyu mdogo wa thamani ambaye, machozi yakitiririka mashavuni mwake, kama tu vile upendo wa mama ungeweza kumwendea mtoto mchanga. Nacho maskini kichwa chake kilikuwa kimevimba sana hivi kwamba, maskini macho yake yalitokeza, mishipa mikubwa mno juu ya kichwa chake, na namna fulani ya sindano ambazo ilimbidi daktari kumdunga kila siku, kusudi apate kuishi siku hiyo yote.

Nami nilipokuwa nikipitia pale, niliangalia hapo na kumwona huyo mama pamoja na maskini mtoto huyo, ndipo nikamwambia Billy, mwanangu, “Maskini jamaa huyo!”

Naye akasema, “Na, Baba, yeye aliniomba kadi ya maombi.” Kisha kasema, “A—alikuwa amechelewa kupita kiasi, tayari nimezisambaza zote.”

Nikasema, “Vema, waambie tu waimbe huo wimbo tena, na, *Amini Tu*, na hebu nifanye hima nikamwombee huyo mtoto mchanga.”

³ Ndipo nikashuka nikaenda na kumwombea maskini huyo jamaa na kumwomba Bwana wetu amrehemu. Ndipo huyo mama akampeleka maskini jamaa huyo nyumbani usiku huo, ndipo kesho yake asubuhi alipoamka, alishangaa, kumtazama jamaa huyo mdogo, ile mishipa mikubwa ilikuwa imekwisha, kichwa kilikuwa cha kawaida kabisa.

⁴ Kwa hiyo mara moja akampeleka kwa daktari, naye daktari akashangaa sana, kisha akasema ilininii. . . alichunguza damu yake, ama chochote walichopaswa kufanya kusudi. . . kwa ajili ya sindano hii, “Mbona,” kasema, “haihitaji tena!”

⁵ Nayo i—ikasababisha vurugu kubwa kote nchini. Ushuhuda mwingine tu kwa utukufu wa Mungu, kujua ya kwamba Yeye—Yeye hujibu maombi wakati mioyo ni miaminifu na inataka kumwamini Yeye. Hakuna jambo kubwa sana Kwake kufanya, nami ninaamini ya kwamba Yeye anapenda tu kufanya hivyo kwa ajili ya watu Wake.

⁶ Sasa, watanipa lundo la haja, katika dakika moja tu, kwa wale waliopiga simu, na, wapate kuombewa. Nanyi huko nje kwenye—kwenye nchi ya redio, ninawatakeni muwe tayari, na kuwa katika matarajio, na muwe na subira hata mtaishikilia ahadi ya Mungu, kwa sababu kuomba kwa imani kutamwoko a mgonjwa yule, naye Mungu atawainua; hayo ni Maandiko.

⁷ Na laiti mngaliweza tu kusimama katika mazingira haya ya Kimbinguni ninayosimamia asubuhi ya leo, hapa kwenye Mkahawa wa Clifton, ambapo kweli kuna mamia ya watu wamesongamana hapa, waaminio wote wanaoamini na wataungana nami katika maombi kuwaombea ninyi pamoja na wapendwa wenu! Chochote kile, kwa nini usilishikilie mbele za Mungu sasa na kuamini ya kwamba Mungu atatusikia na kujibu maombi?

⁸ Sasa, huna budi kuendelea na imani uliyo nayo unapohisi Uwepo wa Bwana uko pamoja nawe. Sasa, watu wengi wanashangaa ni kitu gani kinachotukia wakati wao, wanaonekana kana kwamba wameponywa, halafu baada ya kitambo kidogo hawajisikii hivyo. Lakini ni kwa sababu kwamba wakati maombi yanapofanywa, na Uwepo wa Bwana ukiwa pamoja nawe, imani inapanda juu, halafu imani inapoondoka, vema, basi wewe, jambo fulani limekupata. Huna budi kubaki na imani hiyo, kamwe usiache hisia hiyo ikuache. Sikuzote kumbuka tu ya kwamba Mungu amejibu, ni Neno Lake, kamwe hawezi kulighairi Hilo, hana budi kutimiza Neno Lake. Tena himizo kwako, ukijua ya kwamba Mungu alitoa hiyo ahadi. . .

⁹ Nami ninaamini ya kwamba Biblia ni Mungu katika umbo la maandishi. Tunajua ya kwamba “Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu.” Basi *Hizi* ndizo ahadi Zake, alizotupatia sisi, nasi hatuna budi kuzithamini.

¹⁰ Na sasa, kuna Kitu kimoja tu kitakacholiuisha Neno hili, hicho ni Roho Mtakatifu, huifanya Mbegu Hai. Ndipo wakati ninii, anapoimwaga Roho Yake juu ya nchi, kama alivyofanya katika siku hizi za mwisho, aina yoyote ya mbegu inayomwagikiwa na Roho, ambayo ni maji, kama tu vile, Kristo alipigwa, kama ule mwamba nyikani kwa watu waliokuwa wakiangamia ambao walikuwa wakifa, wakihitaji maji, Kristo alipigwa kusudi wao wamwagiliwe maji ya Uzima.

¹¹ Sasa, kusanyiko, laiti ninyi mlio kwenye nchi ya redio mngeweza tu kuona, wanasimama sasa. Iweni tayari sasa kwa ajili ya maombi, wekeaneni mikono mmoja juu ya mwenzake, juu ya redio, ama mahali ambapo wewe ni mgonjwa, halafu hebu tuombe pamoja.

¹² Baba yetu wa Mbinguni mwenye Rehema, tunapokaribia kiti Chako cha neema sasa katika Jina hilo litoshelezalo kwa yote la Bwana Yesu, nasi tunakuja tukiamini na kuweka maombi yetu na imani yetu madhabahuni pamoja na hawa wote hapa kwa wale walio nchini ambamo wao ni wagonjwa na wahitaji asubuhi ya leo. Baba wa Mbinguni, inaonekana kama Matendo 4 nyingine, wakati watu walipoomba jengo lilitikisika mahali walipokuwa wamekusanyika, nazo nguvu za Mungu zikafanya kazi juu ya watu.

¹³ Shetani na amwachilie kila mtu aliyefungwa katika nchi ya redio, asubuhi ya leo, anayesikiliza. Jalia kuwe ma—matokeo makubwa sana kati yao, mpaka itakuwa kama huo ushuhuda ambao tumetoa hivi punde kuhusu mtoto mchanga mwenye kichwa kilichojawa maji. Jalia kila ugonjwa uwaondokee watu. Jalia nguvu zilizomfufua Yesu katika wafu, na zimemwasilisha kwetu akiwa hai baada ya miaka elfu mbili, jalia nguvu hizo zimhuishe kila mgonjwa na kuwapa afya.

¹⁴ Tujalie, Baba. Tunawakabidhi Kwako, sasa, pamoja na maombi yetu, huku dhabihu ya Kristo ikitutangulia, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

[Kusanyiko linaimba *Amini Tu*—Mh.] Mara nyingine tena. [Kusanyiko linaimba *Amini Tu*. Sehemu tupu kwenye kanda.]

¹⁵ Maandiko yanasema ya kwamba kutakuwa na mvua ya masika na mvua ya vuli. Vema sasa, neno la Kiebrania, siwezi kulikumbuka sasa hivi, lakini *mvua ya masika* linamaanisha “kupandwa kwa mbegu.” Mnaona? Kwa hiyo Mbegu inapandwa sasa na inapandwa kote kupitia madhehebu haya.

¹⁶ Sasa, Roho anapoanza kushuka katika sehemu hiyo kubwa, atazaa kwa jinsi Yake. Kwa hiyo hebu na tuombe ya kwamba Ro—Roho Mtakatifu atapanda Mbegu kote katika shirika hilo, hata lile bubujiko kuu litakapokuja kutakuwa na mazao yatakayotokea humo. Na tuombe.

¹⁷ Baba yetu wa Mbinguni, mioyo yetu imechochewa asubuhi ya leo kwa mihemko mikuu, kwa sababu ya nafasi hii ya kuwaona watu wakiingia, katika saa hii, wakati Nuru za jioni zinapoanza kuangaza. Jalia nguvu kuu za Mungu zienee kote katika dhehebu hilo la Waadventista wa Sabato, kuanzia viongozi kote kote hadi kwenye lile kanisa dogo sana, jalia wamwagiwe Roho Mtakatifu, Bwana. Jalia waipokee Pentekoste na kusanyiko kubwa la watu kwa ajili ya Ufalme wa Mungu kote katika mataifa. Tujalie, Bwana, kote ulimwenguni. Watie mafuta hawa wa- . . . [Sehemu tupu kwenye kanda. Dada mmoja

ananena kwa lugha, dada mwingine anafasiri. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁸ Asanteni. Sijui niseme nini. Nimekosa maneno. Nimesikia mengi sana mpaka nimeshiba kabisa. Hilo si ni zuri sana? Jinsi ambavyo Bwana wetu. . . Hiyo ni ninii tu. . . Nina furaha sana. Ninaamini nilijisikia kuongozwa kuja hapa asubuhi ya leo. Ni vizuri sana kuwa hapa, tumeketi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu.

¹⁹ Tunashukuru sana kusikia huo wa Ndugu Harold, siwezi kutaja jina lake la mwisho, kwa hiyo itanibidi tu kusema Harold, kusikia jinsi ambavyo Bwana alimwongoza hadi mahali hapo pakuu, na yale wanayofanya.

²⁰ Hakika nitasema jambo hili kuhusiana na jambo hilo, kwamba unapoenda kwenye nchi zingine, hao watu huko, inahitaji Ujumbe wa Pentekoste kuwachochea hao watu, mnaona. Wao—wao wana theolojia yote, na vi—vitini vyote, na kadhalika, bali inawabidi kumwona Mungu katika matendo, hayo ndiyo yanayowavutia.

²¹ Wito mmoja wa madhabahuni huko Durban, mkutano wangu wa mwisho kule, tulirekodi watu elfu thelathini waliomjia Kristo, hao walikuwa makafiri watupu, wakati mmoja, mnaona, kwa sababu waliona kitu ambacho wangeweza kushika kwa mkono wao.

²² Ningetaka kusema ya kwamba, kuhusiana na hilo, yule mmishenari mashuhuri huko India, Hudson Taylor, kulikuwa na m—mvulana mdogo wa Kichina aliyekuja asubuhi moja na kusema, “Dk. Taylor,” akasema, “Ndio kwanza nimpokee Kristo moyoni mwangu, na nafsi yangu inawaka moto kwa Roho wa Mungu ndani yangu.” Kasema, “Nisome. . . ? Niende shule gani, kusoma na nipate B.A. yangu?” na kadhalika namna hiyo.

Bw. Taylor akasema, “Usingoje mpaka mshumaa umeungua nusu ndipo uonyeshe nuru.”

²³ Hiyo ni kweli, nafikiri hivyo pia. Wakati. . . Hiyo ndiyo shida, watu hungoja, nao wanawapeleka kwenye seminari hizo na kuondoa yote ambayo Mungu aliweka ndani yao, mnaona.

²⁴ Na—nafikiri, “Nenda mara tu mshumaa unapowashwa.” Kama hujui zaidi, waambie jinsi ulivyowashwa, hayo tu ndiyo inawabidi kujua. Wa—wa—waambie tu jinsi Moto ulivyoanza, na uwaache washike Moto. Mengine yote yatajishughulikia. Ne—nenda tu, waambie jinsi huo mshumaa ulivyowashwa, kisha uwaache wawashwe, nao watamwambia mtu mwingine. Basi, wakati wa kuwasha mshumaa sasa, hiyo ni kweli, hiyo ni kweli.

²⁵ Sasa, ningekuwa mjinga kujaribu kuhubiri nyuma ya kitu kama hicho, mnajua hilo.

26 Kama vile nilivyokuwa hapa juu wakati mmoja kwenye shule nzuri, ndipo mtu fulani akasema, “Ndugu Branham, umeandika vitabu vichache, ningependa kukupa digrii ya udaktari.”

Nikasema, “Mimi ni mwerevu kupita kiasi kwa hilo.”

Kasema, “Kwa nini uwazie hivyo?”

27 Nikasema, “Sasa, wanajua maskini njia yangu ya kuzungumza ya Kentucky, *ake* na *hasina* na *tote*, nami ningezungumza hivyo, halafu niseme ati nilikuwa ‘daktari’? Watu wana akili bora kuliko hiyo. Kwa hiyo mimi ni mwerevu mno kufanya hivyo.” Kwa hiyo tunajua uwezo wetu.

28 Lakini ni vizuri kuwa hapa, kundi hili zuri. Na wakati tu nilipokuwa nikisikiliza ke—kengele za shangwe zikilia katika kila moyo, Andiko dogo lilikuja niani mwangu ambalo huenda nikatumia kwa ninii tu, nasema kwa dakika kumi na tano ama hivi, karibu hivyo, ndugu. Yeye. . . Hakika ninajisikia duni, na kumwomba Ndugu Harold msamaha. Nilishuka hapa asubuhi ya leo kwenye wakati tu aliokuwa azungumze, na halafu, juu miongoni mwa watu, ndipo basi wakanipigia simu nije hapa, ninajisikia vibaya sana, na kumwomba Ndugu Harold msamaha. Mimi. . . [Ndugu Harold anasema, “Naweza tu kusema jambo fulani kwa njia hiyo.”—Mh.] Naam, unaweza kulisema. [Ndugu Harold anazungumza na kusanyiko.]

Unyenyekevu ndio njia ya mafanikio. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli.

29 Ninawaalika huko chini kwenye mkutano usiku wa leo, huko chini kwenye, nilikuita Ikulu ya Ngombe na kumfanya kila mtu kuchanganyikiwa. Mimi. . . Wakati mmoja waliniambia ilikuwa ni Ikulu ya Ngombe, nami nikaona hiyo ni huko San Francisco. Ati wasemaje? Viwanja vikuu vya Maonyesho vya Magharibi. Nasi tuna wakati mzuri sana kule chini, kundi la ndugu, sisi ni kama tu, vema, kama picha ndogo niliyoona wakati mmoja.

30 Nilikuwa huko kaskazini-magharibi, nikivua samaki, nami nilikuwa na ugwe mkubwa wa. . . wengi wenu ninyi ndugu wavuvi hapa. Nami nilikuwa nimebeba mgongoni mwangu kihema cha mbwa, nami nilikuwa huko juu kabisa milimani, na nilikuwa na kihema kidogo na baadhi, mwajua, vifaa. Basi nilikuwa nikivua samaki wa mtoni, nami ningewakamata tu wa kutosha kula, na halafu ninawaachilia hao wengine. Nami ninapenda tu kuvua samaki kwenye kijito hicho kidogo.

31 Basi nilikuwa na mfuko kifauwongo nyuma yangu ambao ulikuwa ukiushika ugwe wangu wakati wote. “Asubuhi,” nikawaza, “vema, nitashuka niende nikachukue kishoka changu, na kuikata hiyo mifuko kifauwongo,” ili maskini Coachman wangu usishikwe kwenye—kwenye hiyo mifuko.

32 Nami nikaondoka kwenye hicho kihema, nikashuka, nikaifyeka, ndipo nikachukua maskini shoka langu,

nikawakamata samaki wangu, kisha nikarudi, kumbe maskini mama dubu na watoto wake walikuwa wameingia kwenye hema langu, nao wakalirarua lote vipande-vipande.

³³ Na kwa hiyo, dubu ni kama tu, na, mlisikia juu ya dubu katika kabati la kichina, si kile wanachoharibu...si kile wanachokula, ni kile wanachoharibu. Nilikuwa na stovu ndogo ya bomba, naye alikuwa tu ameipondaponda hiyo kabisa apate tu kusikia ikichacharika.

³⁴ Na kwa hiyo, niliona...Nami ni—ninapenda...Sasa, yupo mtu yeyote hapa kutoka Kentucky? Ninapenda magole, mwajua. Hizo...Mnaziita chapati maji hapa, naamini. Na kwa hiyo, nami na—napenda kuzipaka sukari ya rojorojo. Na—na mimi—mimi—mimi si...Sinyunyizii, mimi hubatiza, kwa hiyo kweli mimi huzimwagilia, mwajua, kwa hiyo nilikuwa na sukari nyingi—nyingi ya rojorojo.

³⁵ Na—na jambo la kushangaza nilipokuja, maskini huyo mama dubu alikimbia upande mmoja, naye akawaita hao watoto, ndipo mtoto mmoja mdogo akatoroka pamoja naye. Maskini mtoto huyo mwingine akaketi tu pale, alikuwa amenipa kisogo, jamaa wadogo, ilikuwa kwenye majira ya kuchipua. Nami ni—nilijua vema kuliko kumkaribia jamaa huyo mdogo sana, kwa sababu huenda mama akanikwaruza. Kwa hiyo mimi—mimi... Akaendelea kumwita, nami nikaona, “Kwani maskini jamaa huyo ana shida gani?”

³⁶ Ndipo nikaangalia kote, naye alikuwa ameinamisha kichwa chake kabisa namna *hii*, mwajua, alikuwa akiusogeza mkono wake juu chini. Nikawaza, “Kwani ana nini?” Nikazunguka-zunguka, daima nikiuwazia mti, ili nipande mtini kabla hajanifikia, nami nikazunguka, kumbe maskini jamaa huyu alikuwa amechukua kopo langu la sukari ya rojorojo, naye akafungua ninii...ninii chake...kifuniko chake, wala hakujua, bila shaka, jinsi ya kuinywa, naye angeingiza tu maskini unyayo wake namna *hii*, na kuulambia usoni mwake namna *hiyo*, mwajua. Nao wanapenda vitu vitamu. Naye alikuwa sukari ya rojorojo kuanzia kichwani mwake hadi chini ya miguu yake. Naye angeiramba.

³⁷ Ndipo nikapaza sauti, “Toka hapo.” Naye hakunijali hata kidogo, naye mama yake akamwita, bado hakumjali. Nikawaza, “Vema, amepata kitu kizuri sana.” Kwa hiyo alipoangalia pande zote, asingeweza kuyafungua macho yake, amejaa tu sukari ya rojorojo, mwajua, maskini jamaa mdogo anayeonekana wa kuchekesha sana.

³⁸ Nami nikawazia, “Naam, hakuna hukumu kwa hao walio uwanjani, hilo ni jambo moja hakika.” Nikawazia, “Ni kama tu maskini mkutano halisi wa Kipentekoste,” kama vile asubuhi ya leo, tumetia mikono yetu ndani ya kopo la sukari ya rojorojo kadiri tuwezavyo, tukiramba.

³⁹ Mnajua, jambo ni kwamba, wakati hatimaye alipoiangusha ndoo hiyo na kuwakimbilia wale walioogopa kuja pale na kuichukua, hao wengine wakamlamba, hivyo wakilamba hiyo sukari ya rojorojo.

Kwa hiyo hilo karibu ndilo tumekuwa tukifanya asubuhi ya leo, kulamba sukari ya rojorojo kutoka kwenye shuhuda hizi.

⁴⁰ Nimefurahia ushuhuda wa Dada Shakarian. Na maskini huyu Stevie, jinsi alivyokulia hapa! Nilikuwa nikimpigapiga kichwani, na sasa anaweza kunipigapiga kichwani. Sasa, amekua, akawa mvulana mzuri hivi, na kufuata katika...si ajabu, ana msingi mzuri, kitu fulani nyuma yake.

⁴¹ Ninamwona Ndugu Demos hapa baada ya haya yote, na Ndugu Williams, na loo, wengi sana hapa. Sijui tu jinsi ya kusema, lakini ninashukuru kuwa hapa, wakati huu mzuri wa ushirika. Na hapa ni mahali ambapo ni pa Kimbinguni tu kwangu, kuketi tu pamoja namna hii na kuwa na furaha kuu.

⁴² Sasa, kama tulivyoshangilia, waweza...? Kitu fulani kilingia niani mwangu dakika chache tu zilizopita, Maandiko fulani. Na kabla tu hatujayaandea Maandiko hebu tuombe tu, kwa muda kidogo tu.

⁴³ Baba Mungu mwenye rehema, tunakuja katika Uwepo Wako sasa, kwa njia ya neema, kwa agizo la Bwana wetu akisema, “Mwombeni Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya.” Nasi tunajua ya kwamba tutapewa. Tunakushukuru kwa ajili ya kusanyiko hili, leo hii, kwenye chumba hiki cha juu.

⁴⁴ Loo, laiti ulimwengu huu kipofu ungeweza tu kuona na kuhisi ile furaha, kila mlevi angetoka kichochoroni. Ee Mungu, laiti wangelijua furaha ya kweli ni nini! Wanajaribu kuchukua na kunywa, na wengi wamelala kwenye fuo za bahari, na katika kumbi za dansi, wakijaribu kubadilisha kitu fulani na furaha hii kuu ambayo Mungu aliwaleta duniani wapate kuipokea. Mungu, ninaomba ya kwamba kutakuwa na Nuru itakayoenenda kutoka hapa leo, ambayo itawaleta wengi katika maarifa haya yaokoayo na furaha ya Mungu iwe mioyoni mwao.

Asante, Baba. Ninapoyanukuu Maneno haya machache, yabariki kwa kuiendeleza ibada. Katika Jina la Yesu. Amina.

⁴⁵ Katika Kitabu cha Isaya, ningetaka tu kunukuu kutoka kwa kimoja, kwa ninii tu, kwa dakika chache tu, Isaya 32:2, “Na Jina la Bwana ni Ngome imara. Yeye ni Mwamba katika nchi yenye uchovu, Kimbilio wakati wa dhoruba.”

⁴⁶ Ningetaka kuwazia jambo hilo, “Mwamba katika nchi yenye uchovu.” Sasa, kuona kundi hili kwa namna fulani linanikumbusha jambo fulani, hiyo ni kusema, ningetaka kusema jambo hili, ama nitumie *somo* hili, kusema hivi: *Kutoa Presha*. Nafikiri hilo ndilo lililotukia asubuhi ya leo.

⁴⁷ Mnajua, ulimwengu umekumbwa na presha. Kila kitu kinaenda kwa mwendo mkali mno, wala hawajui wanakoelekea. Wanashuka barabarani mwendo wa maili tisini kwa saa, wakasimame kwenye mkahawa wanywe pombe saa mbili kabla hawajafika nyumbani. Na inaonekana tu kuwa ni presha kubwa sana, kila mtu anaudhika kwa urahisi, akisukuma, akibuburusha. Nami na—nashangaa tu tiba yake ni nini.

⁴⁸ Halafu ninakumbuka siku chache zilizopita, mchungaji wetu, nilikuwa nimeingia, nami nilikuwa nimechelewa kwa miito yangu, nao watu wakikusanyika, mwajua, kimataifa kote kule, huku wameketi kwenye hoteli, na moteli na kadhalika, wakingoja, na halafu mchungaji alikuwa amechoka, hakuweza kutekeleza baadhi ya miito ya wagonjwa wake, na baadhi yake ilikuwa ya dharura. Kwa hiyo nikachukua baadhi yake na kwenda kwenye ule, ho—hospitali ya mjini.

⁴⁹ Na ninii, chumba, 331 ninaamini, ilikuwa ndiyo namba, nilikuwa nimwendee mwanamke aliyekuwa afanyiwe u—upasuaji. Basi nikashuka kwenda kwenye 331, naye mwanamke huyo hakuwako. Kwa hiyo nikarudi juu, naye nesi alikuwa amesimama pale akipigapiga mguu wake, nami nikasema, “U hali gani?” Nikasema, “Waweza kuniambia mahali Binti *Anayeitwa hivi* alipo?” Nikasema, “Anapaswa kuwa katika 331.”

Akasema, “Vema, kama anapaswa kuwa katika 331, ndiko aliko.”

Nikawaza, “Loo, jamani!” Nikasema, “Naam, mama. Asante.”

Nikarudi kwenye 331 tena nao wakasema, “Vema, ni, labda ni 332, upande ule wa ukumbi.”

“La.”

Kasema, “Hayupo hapa. Huenda ilikuwa ni 231.”

⁵⁰ Kwa hiyo nikashuka vipandio, na kulikuwa na maskini daktari mmoja ameketi pale kwenye dawati, mtu mdogo, wa kwanza niliyepata kumwona akiwa mpana kadiri alivyokuwa mrefu. Kwa hiyo alikuwa ameketi pale kwenye ubao wa kubadilishia, nami nikapitia hapo, nikasema, “U hali gani?” Akaniangalia tu kiajabu, nami nikawazia, “Uh-uh, sitaki kumwuliza.”

⁵¹ Kwa hiyo nikashuka, chumbani, na kulikuwa na mama aliyekuwa akitoka kwenye chumba cha upasuaji, mama aliyekuwa na barakoa usoni mwake, na—na, nesi pale sakafuni, akaenda kwenye dawati, nami nikasema, “Mama, kidogo nimechanganyikiwa.” Nikasema, “Nilipanda ghorofani kumwona mama mmoja huko 331, naye hakuwepo. Wala nisingeweza kupata... Walisema labda yuko kwenye—kwenye 231.”

Akasema, “Vema, basi, angalia katika 231.”

Nikasema, “Vema, asante. *Jamani!*”

⁵² Singeweza kupata 231. Kwa hiyo nikaanza kushuka ukumbini, naye maskini yule daktari alikuwa akitembea ameshika stethoskopu yake mkononi mwake, akiizungusha *hivi*. Nikasema, “Habari za jioni, bwana.” Nikasema, “Ninatafuta 231. Waweza kuniambia?”

Akasema, “*Hivi na vile.*”

Nikasema, “Asante kwa taarifa yako.” Ni kitu gani?

⁵³ Nikarudi, na kulikuwa na mama mwingine aliyeketi kwenye dawati, nami nilifikiri alionekana mtulivu sana, kwa hiyo nikasema, “Mama, unaweza kuniambia...?” Nikamsimulia hadithi yangu. Nikasema, “Nimechanganyikiwa kidogo. Mimi ni mhudumu, nipo hapa kutekeleza wito.”

Akasema, “Hebu kidogo, bwana.” Akaenda pale, akaangalia kwenye kitabu, kasema, “Naam. Nenda moja kwa moja pembeni. Yeye yuko . . . naye yuko katika chumba 241.”

Kwa hiyo nikawaza, “Vema, Mungu asifiwe!” Mtu mmoja alikuwa ametoa presha. Mnaona?

⁵⁴ Ni presha tu iliyopanda. Ni wakati tunaoishi, wakati wa fadhaa ambapo watu hawajui la kufanya, wanakoelekea. Nao madaktari hawana jibu kwa ajili yake, kwa sababu madaktari wa akili wanatibiwa na madaktari wa akili, kwa hiyo hawana jibu.

⁵⁵ Lakini jibu lipo hakika, mahali fulani. Tungeweza kulishughulikia kwa saa kadhaa. Lakini nilikuwa tu nikiwazia ya kwamba Mungu analo jibu. Laiti wangeweza tu kuketi mahali kama hapa, inaondoa presha, mnaona, pamoja na watu ambao wame—wameingia katika Umilele. Hatutaingia katika hiyo, tayari tuko ndani yake, mnaona. Hiyo ni kweli.

⁵⁶ Nikizungumza hivi majuzi usiku, sisemi chochote cha maana, lakini wakati mwingine Bwana hunipa kitu fulani, nami ninapokipata, nafikiri ni muhimu sana, kwa sababu Yeye alinipa. Nami nilikuwa nikiwazia ya kwamba (nililizungumzia mkutanoni hivi majuzi usiku.), jinsi ambavyo watoto wa Mungu, wakati mmoja wakiwa watumwa, hawana chakula na wanaishi tu, hali tu waliyokuwamo. Ndipo akaja nabii kutoka nyikani, na kuwaambia kuhusu nchi iliyokuwa imejaa maziwa na asali.

⁵⁷ Na sasa, hawakuwa wamewahi kufika kwenye nchi hiyo, hawakujua lolote kuihusu, bali walimfuata. Hatimaye, wakafika Kadesh-barnea, na huko Yoshua, yule shujaa mkuu, likimaanisha Yehova-Mwokozi, akavuka Yordani, na kuleta ushahidi kwamba nchi hiyo ilikuwako. Ambako mwanadamu angeweza kuishi kwa amani, kulea familia yake, watoto wake, na kuwa taifa, na Mungu angewabariki. Na jinsi ambavyo alirejesha ushahidi kwamba Mungu hakuwa amewadanganya

hao watu, ya kwamba hiyo nchi ilikuwako. Nayo ilikuwa nchi nzuri, ilikuwa imejaa maziwa na asali. Walileta kichala cha zabibu ambacho watu wawili walibeba.

⁵⁸ Ndipo, baada ya kitambo kidogo ilimbidi mwanadamu kufa bila shaka, akiisha kuishi na kuwalea watoto wake ilibidi aingie makaburini. Hatimaye, nchi hii kuu ikawa ninii...ubavuni mwote mwa vilima ama, ubavuni mwa vilima vingi, nilipaswa kusema, ukawa ni makaburini, nao waliobarikiwa walilala kwenye makaburi haya.

⁵⁹ Ndipo akaja Shujaa mwingine mkuu wakati mmoja, Yesu wa Nazareti, Yehova aliyefanyika mwili akiishi miongoni mwetu. Naye akashuka na kutwambia ya kwamba “Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi. Ingawa mna nchi mnayoweza kujenga makazi yenu, na kuwalea watoto wenu, na kukuza mazao yenu, na...lakini kuna Nchi ambako mwanadamu hafi, ambako haiwabidi kuzeeka na kufa.” Na Yeye alikuwa ndiye Yohana katika ninii yetu...kwa ajili yetu, Naye akafika Kadeshi-barnea Yake, kiti cha hukumu, ambapo Kadeshi ilikuwa ni kiti cha hukumu, na hapo, Kwake Kadeshi-barnea ilikuwa ni Kalvari, ambapo alizibeba dhambi zetu zote.

⁶⁰ Ndipo akavuka, kile tunachoita, Yordani, mauti, na akarudi kwenye asubuhi ya Pasaka, akituletea ushahidi kwamba mwanadamu anaweza kuishi baada ya kifo. Ndipo akarejesha vishada vya zabibu pia, Naye akawaambia kama wangengejewa kule hata Siku ya Pentekoste...Wote waliziuma, na wakapata u—ushahidi kwamba mwanadamu ni—ni...anaweza kuishi tena.

⁶¹ Nasi tunaishi tena, tumefufuka kutoka katika mambo ya mauti kuingia katika Uzima mpya, na sasa tayari tumeketi pamoja katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, tayari katika Umilele, kwa sababu tunakuwa sehemu ya Uzima Wake, Uzima wa Milele, nao Uzima wa Milele ni Uzima wa Mungu, wa Mungu, kwa sababu sisi ni wana na binti za Mungu.

⁶² Kila kilichokuwa na mwanzo kina mwisho. Kwa hiyo vile vitu visivyokuwa na mwanzo ndivyo havina mwisho, na hivyo vilikuwa ni Mungu tu. Kwa hiyo tunakuwa sehemu ya Uzima Wake.

⁶³ Wazia jambo hilo, Mungu, kwenye Siku ya Pentekoste, Nguzo hiyo ya Moto ilijigawa na Ndimi za Moto zikawakalia juu yao kila mmoja, Mungu akijigawa Mwenyewe, akijigawa Mwenyewe, miongoni mwa watu Wake. Tunakuwa Uzima wa Mungu Mwenyewe ndani yetu, ndipo tumekufa kwa mambo ya ulimwengu, nasi tumefufuka pamoja na Kristo na tumeketi katika ulimwengu wa Roho, tukiangalia nyuma tulikotoka.

⁶⁴ Inatosha kwamba tungeweza kuwazia hilo, na inatoa presha, inaondoa presha tunapotambua nafasi tuliyo nayo sasa katika Kristo kwa kumpokea Roho Mtakatifu, Uzima wa Mungu

Mwenyewe, neno la Kiyunani, *Zoe*, ambalo linamaanisha Uzima wa Mungu Mwenyewe, ukikaa ndani yako, nawe huwezi kufa kadiri Mungu asivyoweza kufa. Sisi ni wa Milele pamoja na aliye wa Milele, amina, tuingojoea wakati huo mtukufu wa ukombozi wa mwili.

⁶⁵ Na sasa tayari tumekufa, na maisha yetu yamefichwa katika Mungu kwa njia ya Kristo na kutiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu. Ibilisi hahusiki kabisa. Na tunapoketi pamoja, namna hii, katika ulimwengu wa Roho pamoja na Kristo, ndani Yake, basi bila shaka tunaweza kutoa presha.

⁶⁶ Ninachukua kwa mfano usiku ule mkuu huko chini Misri, kile sisi sote tunachowazia, ule usiku mkuu wa Pasaka, wakati ambapo Misri yote ilihangaishwa. Kila mtu alikuwa akikimbia nyumba hadi nyumba, na kupiga mayowe kila mahali, bali Israeli wangeweza kuketi wametulia tu katikati ya shida. Walikuwa na jambo moja la kufanya, kupaka damu kwenye kizingiti, na hapo, ungeweza kupumzika kwa utulivu. Na kama Israeli wangeweza kuiangalia hiyo nguzo kwa damu iliyopakwa, na kujua ya kwamba mauti yatapita (Hiyo ilikuwa ni Damu ya Mwana-kondoo katika mfano.), ni zaidi sana vipi tunavyoweza kuwa na hakika wakati Mungu...?

⁶⁷ Sio kuna dhidi ya ndugu zangu Wabaptisti, kama ndugu huyo alivyosema sasa hivi, walisema, “Tunampokea Roho Mtakatifu tunapoamini.” Paulo alisema, “Je, mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?”

⁶⁸ Ndugu mashuhuri wa Kibaptisti alikutana nami si muda mrefu uliopita, naye akaniambia, akasema, “Ndugu Branham, wewe ukiwa Mbaptisti,” akasema, “hilo—hilo linasikika lisiloaminika kwako kusema kwamba hatumpokei Roho Mtakatifu tulipoamini.” Akasema, “Ibrahimu alimwamini Mungu naye akahesabiwa kwamba ana haki.”

⁶⁹ Nikasema, “Ndipo Mungu akampa muhuri wa thibitisho. Alikuwa amepokea imani yake, wakati alipompa muhuri wa tohara, kwa hiyo, tohara sasa ndiyo Roho Mtakatifu. Anaitahiri moyo yetu, na kujua tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Tumefufuka pamoja na Kristo katika ufufuo.” Nikasema, “Sasa, tunapojua jambo hilo, tunaangalia nyuma maishani mwetu na kuona kile tulichokuwa.”

⁷⁰ Kama watu weusi wako hapa, samahani kwa usemi huu, lakini yule mama mweusi aliyetoa ushuhuda mkutanoni wakati mmoja, alisema, alisimama na kutoa ushuhuda wake, akasema, “Vema, nataka kusema hivi,” akasema, “Mimi si—siiko jinsi ninavyopaswa kuwa, wala siiko vile ninavyotaka kuwa. Halafu tena, najua siiko jinsi nilivyokuwa.” Basi hilo lilikuwa—hilo lilikuwa ndilo lenyewe.

⁷¹ Kwa hiyo tunajua ya kwamba tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani kwa sababu tuko hai, hatuko jinsi tulivyokuwa.

Loo, ni ajabu kujua ya kwamba presha inaweza kutolewa, hivyo tu. “Jina la Bwana ni Ngome imara ambayo wenye haki huikimbilia. Naye ni Mwamba katika nchi yenye uchovu,” Mwamba katika nchi yenye uchovu.

⁷² Siku moja nilikuwa nikisoma juu ya tai mashuhuri. Nilihubiri wakati mmoja katika mkutano wa tai, kwa sababu njia pekee ni juu kuzungumzia ni kuangalia maumbile, na Mungu anaishi katika maumbile, kumwangukia tai, kuona tabia zake. Na juu kwenye hekalu hapa juu, nikihubiri juu ya *Mwana-Kondoo Na Hua*, asili yao. Basi mnaona, mambo hayo yote ni Mungu akinena nasi.

⁷³ Basi kuna aina moja ya tai (Wako aina arobaini mbalimbali, maana yake ni “mwenye kurarua kwa mdomo.”), naye tai huyu, anapozeeka, kuna gamba linalotokeza juu ya kichwa chake. Naye anazeeka, karibu anakuwa kipofu, na ni vigumu kwake kutembea.

⁷⁴ Basi hatimaye, anachoka, na manyoya yake yote yanalegea kwa hiyo hawezi kuruka juu sana tena, ndipo anaruka anaenda mpaka, anaruka juu milimani mpaka anaona mwamba fulani. Hapo anaketi kwenye mwamba huo sasa, jukumu ni kwamba inambidi kukigongesha kichwa chake kwenye mwamba huo mpaka gamba hilo ling’oke. Nao wanasema atakigongesha na kukigongesha mpaka kichwa chake kitatokwa na damu, karibu azimie. Atarudi na kukigongesha tena mpaka ganda lote limeng’oka.

⁷⁵ Wakati gamba hilo lote linapotoka kichwani mwake, ingawa anatokwa na damu na amejeruhiwa, analo hakikisho. Atainuka na kupigapiga manyoya yaliyosalia na kupiga mayowe, anatoa presha. Kwa nini? Anajua mara ganda hilo lote likiisha, atafanya upya uhai wake tena. Anafanywa upya tena, uhai mpya hakika utakuja wakati gamba lote limetoweka.

⁷⁶ Ndipo ninapowazia kile...jinsi Mungu alivyo mkuu kumjali tai Wake, kumpa huyo tai njia ya kufanya upya uhai wake anapokuwa mzee, jambo pekee analopaswa kufanya ni kuligongesha hilo ganda ling’oke, hilo ni jambo kuu. Lakini loo, ninajua Mwamba mwingine ambao mtu anaweza kugongesha ganda la ulimwengu Hapo limwondokee, mpaka kila kutokuamini kumeanguka, na kila kivuli na kila pingu imeanguka, mpaka ulimwengu wote umeng’olewa kutoka kwake, kutokuamini kwote kumemtoka, majivuno yote yakamtoka, ugumu wote ukapigwa ukamtoka, ndipo Uhai mpya hakika utakuja. Ndipo unaweza kutoa mvuke na kuanza tu kushangilia kwa sababu Uhai mpya hakika utaibuka, mradi unaweza kuondolea mbali kutokuamini kutoka kwako.

⁷⁷ Kuchukua vitu, na si kuchukua fundisho fulani la sharti, kanuni fulani ya imani, ama kitu fulani ambacho mtu fulani amebuni, chukua tu Neno la Mungu lisiloghoshiwa, na uliamini

na ukae hapo mpaka litakapokuwa halisi kwako. Ninawaambia kuzaliwa upya kunakuja. Hiyo ni kweli kabisa. Tunaweza kutoa mvuke basi, kwa sababu kuzaliwa upya kunakuja.

⁷⁸ Nilikuwa nikihubiri huko juu milimani wakati mmoja, huko Kentucky, nami nikafanya wi—wito wa madhabahuni. Kulikuwako na maskini jamaa mkubwa aliyerudi kule, alikuwa anataka kunitupa nje ya mkutano. Ilikuwa ni wakati wa kukata mahindi, naye—naye alikuwa tu amepasuliwa mguu wa suruali yake, naye alikuwa na msumari ndani yake. Naye alikuwa aende, apande kule na kumtupa nje maskini mhubiri huyu mtakatifu anayejibingirisha. Kwa hiyo wakaniambia alikuwa anakuja.

⁷⁹ Ndipo alipofika mlangoni, wakatili wanne ama watano wakubwa mno, na mikono yao imekunjwa namna *hii*, niliendelea tu kuhubiri. Naye kidogo akangojea kupita kiasi, asingeweza kufika madhabahuni upesi vya kutosha, akaanguka katikati ya sakafu na kuanza kutupa mikono yake juu, akilia, “Mungu, unirehemu mimi mwenye dhambi,” akililia madhabahuni.

⁸⁰ Ndipo basi wakati Roho Mtakatifu aliposhuka na kufunua, na kumwambia yale aliyofanya, akisimama pale, hilo ndilo lililompata. Aliposimama pale, na kumwambia ya kwamba ana mwanamke mwingine aliyekuwa akizurura naye, na huyo hapo mkewe ameketi, na watoto wawili wameketi hapo, na kumwaibisha kwa tendo lile lile alilokuwa amefanya. Alijua ilihitaji zaidi ya mwanadamu kufanya hivyo, ilihitaji Mungu kufanya kitu kama hicho. Ndipo akapiga mayowe, akija madhabahuni, akilia, “Unirehemu, Mungu, mimi ni mwenye dhambi.”

⁸¹ Kesho yake akarudi, akasema, “Ndugu Branham, niliota ndoto jana usiku ya kwamba nilikuwa nikiwatega sungura kondeni.” Naye akasema, “mbwa mkubwa akanifukuza.” Akasema, “Nilianza kukimbia kwa yote yaliyokuwa ndani yangu, wala sikujua niende wapi.” Kisha kasema, “Nikaangalia juu ya mlima, na kulikuwa na jiwe kubwa lenye shimo ndani yake.” Akasema, “Nikawazia kama ningeweza kufika kwenye mwamba huo, ningeweza tu kutoa presha.” Akasema, “Huyo mbwa mkubwa alikuwa karibu sana hata ningeweza kuhisi pumzi yake kwenye visigino vyangu,” akasema, “lakini nilipoingia, niliketi chini na kutoa presha.”

⁸² Hilo ni jambo zuri kufanya. Kuna Mwamba ambamo tunaweza kupata. . . Yeye ni Mwamba katika nchi yenye uchovu, hapo ambapo tunaweza kuketi chini na kutoa presha.

⁸³ Na sasa, marafiki, ni saa tano, nami ninajua tunapaswa kutoka sasa. Nami nina furaha sana kuwa hapa asubuhi ya leo huku presha yote imeondolewa na kuketi miongoni mwa watu kama hawa. Bwana awabariki sana, vizuri sana, na mniombe. Mungu awabariki.

[Ndugu fulani anazungumza na kusanyiko. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Amina. Hilo ni zuri sana.

⁸⁴ Nyote mlisikia ya kwamba hivi majuzi karibu niuawe. M—mlijua hilo, kuhusu kulipuka kwa ile bunduki, moja ya... Bw. Weatherby, hapa chini, alikuwa ametoboa bunduki, nayo ilikuwa ni bunduki iliyotobolewa upya, na ilikuwa ya Winchester. Daima nimetamani Weatherby Magnum, maana nimewinda, na huo ndio mwanya pekee nilio nao.

⁸⁵ Naye Ndugu Art Wilson akampa mvulana wangu ile ya .270, samahani, ni Roberts ya .257, naye Billy hutumia mkono wa kushoto, kwa hiyo asingeweza kuitumia hiyo bunduki, kwa sababu ilikuwa ni komeo tendaji muundo 70, ninyi ndugu mnaotumia bunduki. Na hiyo—hiyo imekuwa ninii yangu...

Mama yangu, mwajua, ndiyo kwanza apenye Mbinguni majuma machache yaliyopita, alikuwa ni nusu Mhindi, nami napenda tu mambo ya nje, na hapo ndipo ninapopigia risasi.

⁸⁶ Nami ni—nisingeweza kamwe... Ninao marafiki ambao wangeninunulia bunduki ya Weatherby. Hiyo ni kweli, ninao. Ila nisingeweza kuwazia kumwacha rafiki yangu aninunulie bunduki ya Weatherby, na kutumia kiasi hicho cha pesa kwake, huku nina marafiki wamishenari ambao wanaenda bila viatu miguuni, nisingeweza kufanya hivyo, la. Kamwe nisingeweza kufanya hivyo.

Kwa hiyo ndugu mmoja akasema, “Nitaipeleka bunduki hiyo itobolewe kwa ajili yako, Billy, nayo itakuwa sawa.”

⁸⁷ Bw. Weatherby akaitoboa. Nilipoirudisha, niliitia risasi, kisha nikaiinua kuipigia risasi namna *hiyo*, ndipo ikalipuka usoni mwangu. Ililipuka ikaurusha mtutu yadi hamsini mbele yangu, nalo shina upande *huu*. Basi yote niliyoona ni moto mwekundu uliofika juu kama dari hii ukipanda juu namna hiyo, nayo damu ilikuwa ikirashia kila kitu. Nami nikainuka kwa amani, nilifikiri nilikuwa nimeaga dunia. Basi lilikuwa ni jambo la ajabu sana.

⁸⁸ Nilipata ujumbe m—mdogo kutoka hapo. Mnaona, bunduki hiyo haikuanza ikiwa Weatherby. Kama ingeanza, hapo mwanzo, Weatherby, ingekuwa sawa, kwa sababu hiyo feleji ingeshikilia. Ili—ilitoa presha kwake. Bw. Weatherby ni mzuri sana, aliipekua hiyo bunduki, asingeweza kujua kilichotukia, lakini nilifikiri ilikuwa ni sehemu ya kichwani iliyolisababisha.

Sasa, mnaona, kama bunduki hiyo ingalianza ikiwa Weatherby hapo mwanzo, na kuendelea, isingalilipuka kamwe.

⁸⁹ Na sasa sikilizeni, enyi marafiki, hebu niwaambieni hili: Unapotoka nje ukikiri Ukristo, usiokote tu wazo lake la kuongoka upya, utalipuka siku moja. Usijaribu kumwiga mtu mwingine, angalia, usijitokeze tu, na kujiunga na kanisa, ama kuimba nyimbo, huna budi kuzaliwa mara ya pili na kuanza

kutoka mwanzo, ndipo utastahimili hiyo presha mradi tu unayo, isije ikalipuka.

Mungu awabariki. Nami ninashukuru ninyi nyote mnaniombea sasa. Mungu awabariki. 🙏

62-0622_B Kutoa Presha
Clifton's Cafeteria
Los Angeles, California Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org